

Na: 15. Msimu wa Kilimo 2017/18 Tathmini ya Kipindi cha Februari 21-28, 2018 na Matazamio kwa Kipindi cha Machi 1-10, 2018


- Wakulima katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua wanaendelea na shughuli za palizi na uwekaji wa mbolea.
- Wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wanaendelea na shughuli za uvunaji wa mazao na kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu wa *Masika*.
- Mvua za msimu wa masika zinazotarajiwa kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua zitasaidia kuongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya kupanda

**MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA
KIPINDI CHA FEBRUARI 20-28, 2018**

Migandamizo mikubwa ya hewa iliyo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo sehemu ya kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika kidogo. Ukanda wa mvua (ITCZ) uliendelea kubaki katika maneo ya kusini mwa Tanzania. Joto la bahari katika maeneo ya kusinimagharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la wastani. Pepo zilivuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine kumekuwepo na joto la bahari la juu kidogo ya wastani hadi chini ya wastani katika eneo la kusinimashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola).

**MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI
CHA FEBRUARI 21-28, 2018**

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, eneo kubwa la nchi limepata mvua za juu ya wastani (zaidi ya 124% ya wastani wa mvua wa muda mrefu kwa siku kumi) kama inavyoonekana kwenye kielelezo. Pia , mvua za chini ya wastani (chini ya 75% ya wastani wa mvua wa muda mrefu kwa siku kumi) zilinyesha katika baadhi ya maeneo ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Kilimanjaro, mashiriki ya mkoa wa Arusha, Manyara, Kagera, Kigoma, katikati ya mkoa wa Morogoro, mashariki ya mkoa wa Lindi na Mtwara pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba.



Kielelezo. Kiasi cha mvua (%) kipindi cha Tarehe 21-28 Februari, 2018.

**TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA
KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2018**

Katika kipindi cha siku kumi zilizopita, maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua, mazao yalikuwa katika hatua ya kuchanua na kutoa maua. Kwa ujumla mazao yalikuwa katika hali nzuri. Wakulima katika maeneo hayo wameendelea na shughuli za palizi pamoja na uwekaji wa mbolea. Kwa upande mwingine wakulima katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua wanaendelea na uvunaji wa mazao pamoja na kuandaa mashamba kwa ajili ya msimu wa mvua za Masika. Hali ya maji na malisho ilikuwa ya

kuridhisha katika maeneo mengi ya nchi isipokuwa baadhi ya maeneo ya mkoa wa Arusha hususan katika wilaya ya Longido.

HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji katika mito viliendelea kuongezeka hususan katika mabonde ya Nyasa na Rukwa kutokana na mvua zinazoendelea.

MIFUMO YA HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA FEBRUARI 21-28, 2018

Migandamizo mikubwa iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kusini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Ukanda wa mvua (ITCZ) unatarajiwa kuanza kupanda taratibu kuelekea kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la juu kidogo ya wastani hadi wastani linatarajiwa katika eneo la kusini-magharibi mwa bahari ya Hindi. Hii inatarajiwa kusababisha upepo kuvuma kutoka kaskazini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kaskazini mwa nchi na kutoka kusini mashariki hadi mashariki katika maeneo ya kusini mwa nchi. Kusinimashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kunatarajiwa kuwa na joto la bahari la wastani hadi chini ya wastani. Hali hii itapelekea upepo kuvuma kutoka magharibi, na kusababisha kuingiza unyevu kutoka Congo kuelekea magharibi mwa nchi. Hivyo kusababisha ongezeko la mvua katika maeneo mengi ya nchi hususan katika siku tano za mwanzo za dekad.

HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2018

Kanda ya ziwa Victoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), na Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa); Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi); Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro): Vipindi vya mvua vitakavyoambatana na

Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba), Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida) na Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora): Vipindi vya mvua zitakazoambatana na ngurumo za radi katika maeneo machache vinatarajiwa.

MATARAJIO NA USHAURI KWA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2018

Mvuua zinazotarajiwa zitasaidia kuongeza unyevunyevu kwenye udongo kwa ajili ya ukuaji wa mazao na malisho. Hata hivyo, unyevunyevu uliokithiri katika udongo pamoja na mvua nyingi vinaweza kuathiri shughuli za palizi na uwekaji mbolea katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua. Kutokana na mvua za masika zinazotarajiwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua hali ya unyevunyevu kwenye udongo inategemewa kuimarika na kuwezesha shughuli za upandaji wa mazao. Maji na malisho kwa mifugo vinatarajiwa kuimarika kwenye maeneo mengi ya nchi. Wakulima, wavuvi, na wafugaji wanashauriwa kupata ushauri wa maafisa ugani husika kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 1-10, 2018

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuongezeka kidogo katika mabonde ya Rufiji, ziwa Viktoria na Ruvuma kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – Barabara ya Morogoro, Dar es Salaam-Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

S.L.P 3056; Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz;

Tovuti: www.meteo.go.tz